# JARIDA MAALUM

Toleo la 17 | Aprili, 2021

## OFISI YA WAZIRI MKUU





# MAJALIWA: SERIKALI ITAENDELEA KUTOA FEDHA ILI KUKAMILISHA MRADI WA UMEME WA MAJI MTO RUFIJI

WAZIRI MKUU, Kassim Majaliwa amewahakikishia Watanzania kwamba Serikali inayoongozwa na Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan itaendelea kutoa fedha za kugharamia mradi wa kufua umeme kwa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) ili ukamilike kwa wakati.

Ameyasema hayo Jumamosi, Aprili 10, 2021 baada ya kukagua mwenendo wa mradi huo, unaotarajiwa kukamilika June 2022. Amesema kuwa Serikali itahakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyostahili.

Waziri Mkuu amesema amefarijika kuona kazi nzuri yenye viwango na ubora wa hali ya juu inayofanywa na Kampuni ya Arab Contractors kwa pamoja na ile ya Elsewedy Electric zote kutoka.... nchini Misri chini ya usimamizi wa TANESCO, TANROADS na Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Majaliwa amesema kukamilika kwa mradi huo kutawawezesha Watanzania kupata umeme mwingi na wa gharama nafuu ambao utasambazwa nchini kote na ziada kuuzwa nje ya nchi ili kulipatia Taifa fedha za kigeni.

Waziri Mkuu amesema bwawa hilo linatarajiwa kuzalisha megawati 2,115 ambazo zikijumlishwa na megawati 1,500 zinazozalishwa na vyanzo mbalimbali nchini hivi sasa zitaifanya Tanzania kuwa na umeme utakaotosheleza mahitaji yake na ziada kuuzwa kwa majirani.

"Lengo la kuanzisha mradi huu ni moja ya juhudi...



Inaendelea Uk. 2



za Serikali za kupunguza gharama za umeme kwa wananchi

kwa sababu uzalishaji wake ni wa gharama nafuu ukilinganisha na vyanzo vingine. Uniti moja ya umeme unaozalishwa kwa kutumia maji inagharimu shilingi 36 hadi shilingi 50 huku umeme unaotumia vyanzo vya mafuta uniti moja inazalishwa kwa gharama ya shilingi 440 hadi shilingi 600."

Gharama/Bei za umeme kwa unit kutokana na vyanzo vingine ni: upepo shilingi 103.5, jua shilingi 103.5, Makaa ya Mawe shilingi 114, Jotoardhi shilingi 118, Nuklia shilingi 65, Gesi shilingi 147.

Waziri Mkuu amesema tayari TANESCO imeshatangaza zabuni ya ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme kutoka kwenye chanzo cha mradi huo hadi Chalinze mkoani Pwani na ukifika Chalinze njia moja itakwenda Dar es Salaam na nyingine Dodoma ili kuwezesha umeme huo kusambazwa nchi nzima.

Kadhalika, Waziri Mkuu ameiagiza Wizara ya Nishati ifuatilie changamoto zote zinazoweza kukwamisha ujenzi wa mradi huo ili kuzipatia ufumbuzi na ihakikishe unakamilika kwa wakati. Pia amewataka wananchi wanaozunguka mradi huo kutoa ushirikiano kwa wajenzi kwa kuwahakikishia usalama wao, mali zao na vifaa vinavyotumika katika ujenzi huo.



# WAZIRI MHAGAMA ATOA MAAGIZO KWA MENEJIMENTI YA OFISI YA WAZIRI MKUU

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mhe. Jenista Mhagama, ameitaka menejimenti na wafanyakazi wa ofisi hiyo kutanguliza taifa kwa kila jambo pia na kuwa wazalendo katika kutekeleza majukumu yao.

Amesema hayo tarehe 9 Aprili, 2021 Jijini Dodoma kwenye kikao kazi na menejimenti ya ofisi hiyo kilichojumuisha wakuu wa idara, vitengo na taasisi zilizo chini ya ofisi hiyo.

"Kila tunachofanya ni kwa ajili ya taswira ya Mhe. Waziri Mkuu na ofisi ya Waziri Mkuu, nasikitika miongoni mwetu tukishindwa kutekeleza wajibu wetu tutatia doa ofisi ya Waziri Mkuu. Katibu mkuu fikiria utaratibu wa kudhibiti uzembe lazima kila mmoja awajibike. Tumepanga katika mambo ya msingi hatutasita kufuatilia utendaji ili kila mmoja atekeleze wajibu wake."Amesema Mhe. Mhagama.

Aidha amewataka kutumia ubobezi wa taaluma walizo nazo ili kuleta matokeo yenye tija kwenye ofisi hiyo kwa kuwa wabunifu katika utendaji wa shughuli zao kwa kuizingatia kasi ya serikali ya... awamu ya sita.

Aidha Waziri ameagiza kabla ya mwisho wa mwezi huu wa Aprili, mfumo wa kielektroniki wa vibali vya kazi na ukaazi kwa wageni uwe umezinduliwa na kufanya kazi ili kudhibiti mianya ya rushwa. Mfumo huo utasaidia kupunguza urasimu wa utoaji vibali kwa wawekezaji.

"Tayari tumesha wafukuza baadhi ya maafisa kazi wanye tabia ya kupokea rushwa kwenye vibali, tunataka mfumo huo kusaidia kuondoa tatizo la rushwa kwenye vibali, tunazo taarifa sisi tukisha pitisha utoaji vibali hivyo vinachukua zaidi ya wiki mbili havijatolewa ili kumfikia muhusika. Nataka mfumo huo uanze kufanya kazi." Amesisitiza Mhe. Mhagama.

Masuala mengine ambayo ameagiza Mhe.Mhagama ni kufuatilia mradi wa kukuza ujuzi, mafunzo ya uwanagenzi, mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi kwa wahitimu, suala la migogoro kwa wafanyakazi kupitia tume ya usuluishi na uwamuzi, masuala ya mawakala kukagua mahali pa kazi.



# KATIBU MKUU NZUNDA AHIMIZA KASI NA MATOKEO OFISI YA WAZIRI MKUU

Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) amewataka Manaibu Makatibu Wakuu wapya, Menejimenti na watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu kuongeza kasi, bidii na ari katika utendaji kazi wa majukumu ili kutoa matokeo yenye tija kwa wananchi.

Katibu Mkuu Nzunda ameyasema hayo Aprili 8, 2021, Jijini Dodoma, wakati wa kuwapokea Manaibu Makatibu Wakuu wapya wa Ofisi ya Waziri Mkuu walioapishwa Ikulu Jijini Dar Es Salaam, Aprili 6, 2021 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Ameeleza kuwa, Ofisi hiyo ina majukumu makubwa ikiwemo kuratibu shughuli za Serikali, hivyo ni muhimu kuongeza nguvu zaidi katika utekelezaji wa majukumu ili kusimamia kwa ufanisi uratibu wa shughuli za serikali.

"Jukumu letu ni kumsaidia Mhe. Waziri Mkuu kutekeleza majukumu ya kusimamia shughuli za serikali, hatunabudi kufanya kazi kwa utaalamu, weledi na kwa kuwajibika kwa kujituma ili kuhakikisha tunapata matokea anayo yataka," alisema Nzunda

Kwa upande wa Manaibu Makatibu Wakuu wapya; Profesa Jamal Adam Katundu na Bw. Kaspar Kaspar Mmuya. wamemhakikisha Katibu Mkuu, kushirikiana na Watendaji wa Ofisi hiyo kwa kufanya kazi kwa kasi na weledi ili kuhakikisha changamoto za wananchi zinapata ufumbuzi kwa wakati.

Tarehe 6 Aprili, 2021 Ikulu Jijini Dar Es Salaam, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan aliwaaapisha Manaibu Makatibu Wakuu wa Ofisi hiyo.

**KATIBU MKUU**
**Ofisi ya Waziri Mkuu**
**2 Mtaa wa Relini, S.L.P 980**
**40480 Dodoma,**
**Baruapepe: ps@pmo.go.tz, Simu:+255262322480**
**Fax:+255262324534, Tovuti: www.pmo.go.tz**